Maulizo juu ya mpango wa mabadiliko ya shule

Mipango/kukamilishwa

Niyaba ya mabadiliko haya ni gani?

Lengo la mpango huyu ni kuwapatiya watoto wote wa Cleveland bahati ya majifunzo bora itakayo faidiya wanafunzi wetu wanapomaliza majifunzo yao ya juu kutoka shule zetu za Cleveland.

- Ku gradiweti wanafunzi wanao kuwa tayari kwa kupingana na uchumi wa senturi ya 21.
- Kuunda shule za majifunzo ya hali ya juu katika kila jumuia na kuruhusu kila jamaa kuchagua shule wazipendazo.
- Kuweka kila mutu kuhusika na mafanikiyo kwa njia ya deta kamilifu;walimu, viongozi, wanafunzi na jumuia.
- Kuwapa kazi,kusaidiya na kubaki na walimu na viongozi wanaofaa.
- Kuendelesha yanayofanyika vizuri na kubadilisha yasiyofanyika vizuri
- Kuvuta na kubakilisha wanafunzi na jamaa hapa Cleveland
- Kukamilisha kazi inayofanyika kwa leo,kwa kutosha visivyofaa na kuhakikisha matumizi bora ya vifaa vya kazi.

Mipango hii itaanzishwa lini?

Mpango huu ni mahitaji ya kuanziliya ya jimbo la shule kwa bodi kuu la elimu hadi itakapokamilishwa na bodi hii.Shule zitakazo fungwa na mabadiliko ingineyo itakamilishwa kwa mwaka wa shule 2010-2011 na itaendeleya kutimilizwa.

Mahitaji hii hayawezi kubadilshwa tena?

Mpango huu ni mahitaji ya mwanzo ya jimbo la shule kwa bodi la elimu,hadi itakapo kamilishwa kiisha uchaguzi utakao fanyika kati ya mwezi wa pili.Jimbo litapokeya taarifa zipya kwa muda wa wiki tatu ao ine ya mwezi wa kwanza kabla mahitaji ya mwisho kupewa kwa bodi.

Mpango huu utatekelezwa kwa mara moja ao kwa vipindi?

Mpango utawekwa kwa vipindi.Mabadiliko ni mpango wa myaka mingi itakayo endelesha usaidizi kwa shule na uchaguzi wa shule na wanafunzi na jamaa kwa muda wote.Mfano ni kama vile shule za chuo kubwa zitakazo anzia kwa mwaka wa tisa(9^{th} grade) wa shule(na ikiwezekana kwa mwaka wa kumi) tangu mwaka wa shule 2010-2011 na zitaongezwa gradi za juu kila mwaka.Ingine mfano ni shule zimoja kwa levo ya chekecheya hadi gradi ya nane(K-8) zitakazopewa usaidizi wa majifunzo tangu mwaka wa kwanza,wakati zingine zitakuwa zikichunguzwa hadi mwaka wa 2011-2012.

Ni je ratiba ya kukamilisha mpango huu?

Mabiliko yatafanyika ndani ya kipindi cha mwaka tano hadi kumi.Kufanikiwa itaomba maono ya muda murefu na lengo kichwani;kukiwa na kukitimilishwa lengo zilizoamuliwa kutimizwa.

Mpango huu utahusu wa nani?

Mageuzo ya vyuo hii ni mabadiliko ya ajabu CMSD imechukuwa kwa muongo huu;mafanikiyo yake itaomba kuunganisha nguvu ya wote katika wilaya hii,

- Wanafunzi kujitowa kwa kutimiza lengo kwa nguvu na kufikiya levo ya mafanikiyo
- Wafanya kazi kujali kila siku kwa yanayohusu zaidi wanafunzi
- Jumuia kusaidiya wanafunzi na kuwa na mahusiano kamilifu na shule
- Wazazi na walimu kuwapa wanafunzi moyo wa tegemeo ya juu

Mpango huu utasawazisha namba za wanafunzi shuleni?

Ndiyo.Kwa levo ya namba za wanafunzi mpango utakuwa kwa kiasi kinachofaa(80-90% ya matumizi ya shule katika jimbo lote la shule)

Ni nani aliyehusika na mageuzo haya?

Washika madau wengi(stakeholders) wa CMSD walihusika na ukamilishaji wa mpango huu.Timu kubwa la CMSD lilitayarisha mpango huu kufatana na mikutano na jumuia mbali mbali,komiti tofauti,timu ndogo la somo za K-8 na viongozi wa sekondari ya juu,hata utafiti kutoka majifunzo ya kundi la Boston Consulting Group kwa mifano ya mipango kama hii iliyofaulu katika jimbo zingine za shule.
CMSD ilifata tena ushauri wa kundi tatu za wachunguzi(council of Great City School on speciality programs/Schools;Education First on turnaround strategies;and BCG on facility utilization)

Mpango huyu utaomba pesa ngapi?

Mpango huu utatumikisha kiasi ya pesa inayokuwa kati ya millioni ishirini na millioni ishirini na tano(20-25millions) kwa kila mwaka kwa kutimilizwa(Karibu 2-3% ya bujeti ya kazi ya CMSD).
Mpango utalipwa kutoka njia tatu:

- Pesa za kuchangiya kutoka kwa serkali
- Miundo ya mtaani na usaidizi wa wafanya vyashara wa jumuia
- Matumizi itayo wekwa kwa pesa zinazotoka ndani ya kazi mbali mbali

Mitihani za shule

Itakuwa je kwa sinia(senior) ambaye shule yake itafungwa ao kuhamishwa?Vyeti vya Diploma yake vitakuwa vya shule alipokuwa akisomeya kwa myaka mitatu iliyopita ao ya shule mupya iliyohamishwa?

Wanafunzi watapewa Diploma za shule waliposomeya kwa mwaka wa ine.

Ni wakati gani wanafunzi wanaosomea kwa shule litakalofungwa ao litakalohamishwa wataombwa kuhamishwa kwa shule mpya?

Kufungiwa na kuhamishwa kwa shule itakuwa wakati wa mapumziko makubwa ya sama(summer) na wanafunzi wataanza kwa shule mpya kwa mwaka wa shule 2010-2011.

Shule wanaposomeya wandugu likafungwa,wandugu hao watatumwa kwa shule wandugu zao wanaposomeya?

Kwa ujumla wandugu wanaojifunza kwa shule zilizokaribiyana wanaweza andikishwa kwa shule moja pamoja.Alakini kwa kuwa wanafunzi wamoja wamoja wanasoma kwa programu tofauti(majifunzo maalamu,lugha ya kingereza…) wanafunzi wanaweza kujifunza mahali tofauti na ndugu zao.Mafasiliyo zaidi juu ya hii yapatikana kwa mitandao ya komputa ya CMSD.

Jimbo la shule litaendeleya na hati lake la wanafunzi kujiandikisha shuleni?

Ndiyo.

Ni je nikaamuwa kutotuma mtoto wangu kwa shule mpya alipotumwa ikiwa shule ninalolipenda halina nafasi?

Ikiwa shule ulilolipenda halina nafasi,mwanafunzi na wazazi wana njia tatu:
1.Jamaa linaweza chagua shule lolote katika wilaya hii
2.Mwanafunzi anaweza kuomba kutumwa kwa shule ingine yoyote ndani ya jimbo linalokuwa karibu ya makao yake.
3.Mwanafunzi anaweza kusomeya kwa shule jirani atakalo chaguliwa na ofisi ya jimbo la shule alilokuwemo
Mafasiriyo zaidi yatapatikana kwa mitandao ya komputa ya CMSD.

Uteuzi wa wanafunzi utafanyika je kwa mpango huu mpya?

Baada ya mpango kukubaliwa na bodi la elimu,jimbo la shule litachunguza kila nafasi wanafunzi walichaguliwa,kwa mwaka 2010-2011 na kila mwanafunzi atajulishwa shule

lake kwa mwaka 2010-2011.Wanafunzi na jamaa watakuwa tena na nafasi ya kuomba shule kati ya shule zingine za mahali walipo ao kuomba kuhamishwa ndani ya jimbo la shule tofauti.Uteuzi wa mwisho utaandikwa na kutumwa pamoja na ripoti kadi ya mwaka wa 2009-1010.

Ni lini naweza jua uteuzi wa shule langu mupya ?

Kila mwanafunzi atazamiye kujuwa uteuzi wa shule lake kwa mwisho wa mwezi wa ine 2010.
Mateuzi ya kwanza yakiisha fanyika wanafunzi na wazazi wanaweza kuomba kuandikishwa kwa shule walipendalo ndani ya jumuia ao kuhamishwa kwa jimbo lingine jirani la makao yao ao kwa shule jirani lililo chaguliwa na ofisi ya jimbo la shule akaamo.Uteuzi wa mwisho utaandikwa kwa ripoti kadi ya mwezi wa sita 2010-2011,wakati masomo yatafungwa.

Usafirisaji

Usafirisaji utapewa kwa wanafunzi watakao hamishwa?

Wanafunzi wa tangu somo la sita na juu wanao makao yao kwa distansi ya zaidi ya mile mbili(3.2km) watapewa usafirisaji wa bus za shule ao tiketi ya RTA Itafanyika hivo kwa wanafunzi watakao someya kwa shule jirani ya inje ya jimbo la shule yao.

Kutakuwa mabadiliko kwa namna ya kupewa usafirishaji?

Hakuna mabadiliko inayoweza semwa kwa wakati huu.

Kuusika/Majibu

Ni njia gain bodi ilifata kwa kukubali mpango huu?

Bodi ilioneshwa kipindi cha mpango huu mwezi wa nane na iliendeleya kujulishwa kwa kila hatua ya matayarisho ya mpango huu.Baada ya usikilizaji wa mafikiri ya jumuia,bodi inatazamiwa kuteuwa mpango huu wa mabadiliko haya kwa mkutano utakao fanyika tarehe 23 ya mwezi wa pili 2010.(23-02-2010)

Kutakuwepo tena mikutano ingine ya jumuia ao nafasi ingine kwa kuhusika na mpango huu ?

Ndiyo.Kutaendeleya mikutano ya jumuia ya masomo mbali mbali.Tarehe zitajulishwa kwa mitandao ya komputa ya CMSD kila wakati kukiwa mabadiliko ao habari mpya yoyote.Mafikiri yanaweza kuandikwa kwa ukarasa wa “Talk to the CEO”(Sema na mkurugenzi) kwa komputa.

Jimbo ao wilaya linatarajiya kufanya nini na majengo itakayo achiliwa na shule zitakazofungwa?

Kipindi 3313.41 cha sheria ya Ohio kinaandika ni hatua gani ya kuchukuwa wakati shule haitumikishwe tena kwa kazi za majifunzo ao za uongozi,wa ghala ao kwa kazi za elimu tofauti.Kwa mwisho wa mwaka wa masomo 2010 majengo yatakayo fungwa yatalindwa kwa usalama.Baada ya mpango wa mabadiliko kukubaliwa bodi itashika sheria, ndani ya mwaka moja ,yenye itatiya mpango unaoelekeyana na shule zitakazofungwa.

Ni usalama na ulinzi gani uliotekelezwa kwa kukamilisha mahitaji

Matekelezo yalikuwa kuhusu shule zinazokuwa na matatizo na mahali zilipo.Msaada zaidi utapewa kwa hizo shule kwa kuongeza hali yazo kwa wafanya kazi sawa vile kwa vifaa vinavyo hitajika.Kiasi cha namba za wanafunzi pia kilitazamiwa na kitabadilishwa kufatana na vile shule litaongezewa wafanya kazi na vifaa vya kazi.

Kazi za usaidizi

Kutakuwa usaidizi kwa muda wa mpito kwa wanafunzi kwa kuzoweya shule mpya?

Ndiyo.Kutakuwa timu ya kusaidiya wanafunzi watokao kwa shule zitakazofungwa.maelekezo ya ajensi za kazi za kijamii zitaweza kupewa pia.

Mtoto wangu atakuwa na walimu wapya ao walimu watahamishwa pamoja na wanafunzi?

Shule zitakazofungwa:Walimu hatahamishwa na wanafunzi.Walimu watapangwa kufatana na kuomba kwao na tena kuhamishwa kufatana na majadiliyano ya umoja wa wafanya kazi wa walimu.Kunaweza kuwa tofauti ya programu,na hapo ndipo itaomba walimu wahamishwe na wanafunzi.